HATI YA MAKUBALIANO

KATI

WANAVIJIJI 17 WA VIJIJI VYA MANG'ONYI NA MWAU

NA

SHANTA MINING COMPANY LIMITED

---

KUHUSIANA NA MALIPO YA FIDIA YA UHARIBIFU INAYOTOKANA NA SHUGHULI ZA UTAFITI WA MADINI KATIKA VIJIJI HIVI MWAKA 2006 NA KUJUMUISHA SHUGHULI ZO ZOTE ZA UTAFITI ZILIFANYWA NA KAMPUNI YA SHANTA MINING COMPANY LIMITED MPAKA DECEMBER, 2014

HATI YA MAKUBALIANO

---

MAKUBALIANO haya yanafanyika leo tarehe 25 Mwezi Feb 2015.

Kati ya

EMIL JOHN MJENGI, ALLY NGADU, JUMA A. HANTI, ALPHONCE MAGUMULA, MAGANGA MUMAA, MIKANURI MSANDAI, MOHAMED ISSA, MATHAYO GHULIKU, BASIL JOSEPH, KATARINA KIMU, BENJAMINI MWAIRIMU, YONA MWAIRIMU,PETRO MWAIRIMU watu binafsi wa Kijiji cha MANG'ONYI katika Wilaya ya IKUNGI , SAMWEL SHABANI, NTUI MWIHILI, SAMWEL LAMECK watu binafsi wa Kijiji cha MWAU katika Wilaya ya IKUNGI na PAROKIA YA DUNG'UNYI (katika mkataba huu watajulikana kama 'Watu' neno hili linawakilisha pia warithi na au wawakilishi wao wa kisheria) kwa upande mmoja;

Na

SHANTA MINING COMPANY LIMITED Kampuni iliyosajiliwa kisheria, yenye leseni ya kufanya utafiti na uchimbaji wa madini katika Wilaya ya Ikungi, Mkoa wa Singida (katika mkataba huu watajulikana kama 'SMCL' neno hili linawakilisha pia warithi na au wawakilishi wao wa kisheria) kwa upande wa pili;

UTANGULIZI

A. Watu walikuwa wamiliki wa ardhi ya kimila katika Vijiji vya Mang'onyi na Mwau katika Wilaya ya Ikungi kama ilivyothibitishwa katika ripoti ya Mkuu wa Wilaya ya Singida (kwa wakati huo) ya mwaka 2006 ambayo ni kiambatanisho "X1" katika makubaliano haya.

B. Watu walitambuliwa na kikosi kazi kilichojumuisha wajumbe kutoka SMCL, walioguswa na eneo la mradi, wanakijiji huru, ngazi ya kijiji, kata, na serikali ya wilaya ambapo majina yao yapo kwenye kiambatisho "X2" katika makubaliano haya.

C. Ambapo [M.PATEL] alikuwa ni mmiliki wa awali wa leseni ya kufanya utafiti wa madini katika maeneo haya. Watu walilalamikia uharibifu uliotokana na shughuli za utafiti huo.

D. Ambapo kufuatia kazi iliyofanywa na kikosi kazi juu utambuzi wa wamiliki pamoja na kufahamu kiasi cha fidia ya uharibifu kwa kila mmoja wao, leseni iliyokuwa inamilikiwa na [M.PATEL] ilihamishiwa kwa SMCL.

E. Baada ya kufanya mashauriano na wadau mbali mbali kwa kutaja wachache ikiwa ni pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Kamishna Msaidizi wa Madini, Mbunge, Mwenyekiti na Katibu wa kikosi kazi, Halmashauri ya Kijiji cha Mang'onyi na Mtendaji Kata ya Mang'onyi, imekubaliwa kwamba SMCL ikishirikiana na [M. PATEL] walipe fidia ya uharibifu kwa walalamikaji kwa viwango walivyokubaliana pamoja na kamati ya maridhiano iliyoundwa kufuatilia swala hili ikijumuisha wajumbe 3 kutoka SMCL, wajumbe 3 kutoka kwa jamii, na Mwenyekiti wa kikosi kazi katika kikao kilichofanyika tarehe 17/12/2014 Ikungi.

F. Katika kikao cha mwisho cha kikosi kazi ilikubaliwa kuwa swala la malipo ya fidia ya uharibifu lishughulikiwe kwanza na kumalizika kabla ya kuendelea na shughuli zaidi za utafiti katika leseni za uchimbaji MLs na utafiti PLs za SMCL na katika mwendelezo wa hatua zaidi za mchakato wa fidia.

KWA HIYO MKATABA HUU UNASHUHUDIA KAMA IFUATAVYO:

1. SMCL italipa kwa watu jumla Tsh. 33,659,640/= [Milioni Thelathini na Tatu Laki Sita Hamsini na Tisa Elfu Mia Sita Arobaini] kama malipo kamili na ya mwisho ya madai yao ya fidia ya uharibifu kuanzia mwaka 2006 hadi December 2014.. Mchanganuo wake umeambatishwa kama "X3"
2. Kwa kuweka saini zao katika makubaliaano haya Watu wanakubali kupokea malipo yao. Kwa kufanya hivi wanakubali kuondoa madai yao ya fidia ya uharibifu dhidi ya M. PATEL, SMCL na WARITHI wao madai ya tarehe 21 September, 2006 kama yalivyoainishwa katika ripoti ya Mkuu wa Wilaya ya Singida 2006.
3. Inakubaliwa kuwa watu ni wamiliki halali na wa pekee wa ardhi tajwa na kwamba kama kulikuwa na haja ya kupata kibali kutoka kwa mtu au mamlaka nyingine kabla ya kufanya makubaliano haya basi Watu wamepata kibali au ruhusa.
4. Endapo ikitokea hapo badae akajitokeza mtu/watu au upande mwingine kudai kuwa mmiliki halali wa ardhi katika maeneo haya itakuwa ni jukumu la mlipwaji/walipwaji wa fidia ya uharibifu kushughulika nao na siyo SMCL.
5. Imekubalika kuwa haya yatakuwa malipo pekee na ya mwisho kuhusiana na swala la malalamiko ya fidia ya uharibifu uliotakana na shughuli za utafiti wa madini zilizofanywa na

M. PATEL, SMCL, na WARITHI wao na kwamba hakutakuwa na madai au malalamiko dhidi ya M. PATEL, SMCL, na WARITHI wao kuhusiana na jambo hili la uharibifu

6. Imekubalika kuwa pande zote zinazohusika na makubaliano haya hazitashitakiana popote au kulalamikiana tena kuhusiana na suala la fidia ya uharibifu au jambo lolote linalohusiana na suala hili la uharibifu
7. Waliotajwa katika UTANGLIZI E wamekubali kuweka saini zao katika makubaliano haya kama mashahidi. Ni uthibitisho wa usahihi wa makubaliano haya.

Hati ya Makubaliano haya imeandikwa katika lugha mbili za Kiswahili na Kiingereza zote zikiwa na jumla ya kurasa 12.

KWA USHUHUDA SISI tunaweka saini zetu katika hati hii leo tarehe.................., Mwezi................. 2015

RHT of Hussein Ally (SON).

| | | |
|---|---|---|
| EMIL JOHN MJENGI | ALLY NGADU | JUMA A. HANTI |
| ALPHONCE MAGUMULA | MAGANGA MUMAA | MIKANURI MSANDAI |
| MOHAMED ISSA | MATHAYO GHULIKU | BASIL JOSEPH |
| KATARINA KIMU | BENJAMIN MWAIRIMU | YONA MWAIRIMU |
| PETRO MWAIRIMU | PAROKIA YA DUNG'UNYI | SAMWEL SHABANI |
| NTUI MWIHILI | SAMWEL LAMECK | |

RHT of Ruhama Mathayo (WIFE)

RHT of Musa N. Mwihili (SON)

NTUNTU PARISH
P.O. BOX 487
SINGIDA

IMETIWA SAINI hapa IKUNGI na SHANTA MINING COMPANY LIMITED
Mbele yetu leo tarehe..25......, Mwezi..FEBRUARY..2015.

SHANTA MINING CO. LTD.
SINGIDA PROJECT
P.O. Box 79408
DAR-ES-SALAAM

MUHURI

Jina:...Z. SWANEPOEL...............

Sanii.........................................

Wdhifa: MENEJA MKUU - SMCL

Jina:..ELISANTE KANUYA.........................

Saini:..............................................

Wadhifa: MENEJA MRADI - SMCL

IMETIWA SAINI hapa IKUNGI na M. PATEK

Mbele yangu leo tarehe........., Mwezi 2015

Jina..................................................

Saini..............................................

Wadhifa..........................................

Anuani:.........................................

MBELE YETU:

MANJU SALUM MSAMBYA
MKUU WA WILAYA - IKUNGI
MKUU WA WILAYA
IKUNGI

TUNDU LISSU 04/03/2015
MBUNGE, SINGIDA MASHARIKI

| | |
|---|---|
| SOSTHENES M. B. MASOLA | MUHAMMAD NKYA |
| KAMISHNA MSAIDIZI WA MADINI | MWENYEKITI KIKOSI KAZI |
| KANDA YA KATI | MWENYEKITI KIKOSI KAZI - MANG'ONYI |
| DAUDI I HUNGU | JUMANNE GWAYE |
| KATIBU – KIKOSI KAZI | MTENDAJI – KATA YA MANG'ONYI |
| KATIBU TAWALA WILAYA IKUNGI | |
| YOHANA NYIKA | ABRAHAM IKAKA |
| MTENDA – KIJIJI CHA MANG'ONYI | MTENDAJI – KIJIJI CHA MWAU |
| AFISA MTENDAJI KIJIJI CHA MANG'ONYI SINGIDA (V) | AFISA MTENDAJI KIJIJI CHA MWAU |